# Mapatano na Maridhiano kwa Umoja wa Wakenya:

# Kutoka kwa taifa la mahusiano ya damu hadi kwa taifa lenye maadili.

**MUHTASARI WA RIPOTI YA JOPOKAZI LA RAIS KUHUSU MAPATANO, MARIDHIANO NA UMOJA WA KITAIFA**

OKTOBA 2019

# Yaliyomo


UTANGULIZI ........................................................................................3

SURA YA 1 — MASUALA MUHIMU..........................................................4

SURA YA 2 — MAADILI YA KITAIFA ........................................................6

SURA YA 3 — MAJUKUMU NA HAKI ZA URAIA ..........................................9

SURA YA 4 — UHASAMA WA KIKABILA NA USHINDANI .............................10

SURA YA 5 — CHAGUZI ZENYE KULETA MIGAWANYIKO...........................12

SURA YA 6 — USHIRIKISHWAJI ...........................................................20

SURA YA 7 — USTAWI KWA WOTE .........................................................22

SURA YA 8 — UFISADI ........................................................................26

SURA YA 9 — UGATUZI ........................................................................28

SURA YA 10 — USALAMA NA ULINZI........................................................32

SURA YA 11 — TUME NA MASUALA YANAYOGUSA KILA KIPENGEE...........35

# UTANGULIZI

Rais Uhuru Kenyatta aliteua Jopokazi la Mapatano, Maridhiano na Umoja wa Kitaifa kupitia kwa Arifa ya Gazeti Rasmi la Serikali No. 5154, iliyochapishwa tarehe 31 Mei, 2018. Ilikuwa fursa ya Jopokazi hilo, kwa mujibu wa mamlaka yake, kutathmini changamoto za kitaifa zilizoorodheshwa katika Mkataba wa Pamoja wa 'Mapatano na Maridhiano katika kujenga Taifa Jipya la Kenya', na baada ya kufanya hivyo, kutoa mapendekezo mwafaka na rai za mageuzi zenye kujenga umoja wa kudumu.

Shughuli hii ilikita mizizi katika kila kona ya nchi hii wakati wa kutafuta maoni: zaidi ya raia 7,000 kutoka makabila yote, jinsia, utamaduni na dini, na sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi zilishauriwa. Jopokazi lilikusanya maoni kutoka kwa zaidi ya viongozi 400 waliochaguliwa wa zamani na sasa; sauti za watu maarufu katika jamii; na kauli za vijana waliowakilisha raia kwenye Kaunti; watu 123 wanaowakilisha taasisi kuu, pamoja na taasisi za kikatiba na wadau wakuu katika sekta za umma na za kibinafsi; watu 261 na mashirika yaliyotuma taarifa kupitia baruapepe; na raia 755 waliotoa mawasilisho yaliyoandikwa kwa mkono wakati wa vikao vya umma katika Kaunti. Jopokazi limewasilisha ripoti yake ya mwisho, ambayo inaonyesha baadhi ya mashauriano ya kina ya raia na wataalamu kuwahi kufanywa na jopokazi kama hili katika historia ya Kenya.

Ripoti hiyo ndio sauti ya Wakenya, na utekelezwaji wake unapaswa kufanywa kwa dhati. Hapa chini kuna vipengee kadhaa kutoka kwa ripoti kamili, ambavyo tunapendekeza visomwe kwa ukamilifu.

# Sura ya 1 — Masuala Muhimu

Wanajopo wa BBI walipokuwa wanazunguka nchini, waligundua matatizo makubwa ambayo yanaathiri suluhisho zilizobainishwa kukabiliana na changamoto maalum. Wanatoa wito kwa kila mmoja kutafakari kwa kina zaidi ikiwa kweli tunataka ufumbuzi wa changamoto zetu zingine ili kujenga Kenya yenye umoja, amani na mafanikio.

1. **TAIFA LA MAADILI DHIDI YA TAIFA LA MAHUSIANO YA DAMU**—Ili Kenya liwe taifa lenye umoja, ni sharti liunganishwe kwa maadili na matamanio ya pamoja wala sio kwa damu na udongo. Taifa lililounganishwa kwa maadili na matamanio ya pamoja hujenga taswira ya matumaini ambayo huboresha mustakabali wa nchi.

2. **VIJANA WANAHISI KUTENGWA** — Wakenya wenye umri wa miaka 15-24 huunda asilimia 20.3, zaidi ya wastani wa asilimia 15.8, na wote wanafahamu kuhusu uwezo wao finyu wa kupata nafasi nzuri za kazi. Idadi na ubora wa kazi zinazopatikana kwa vijana wa Kenya ni chache zaidi ya inavyohitajika.

3. **MUDA UNAZIDI KUYOYOMEA KWA TAIFA LA KENYA** — Wakenya wanajua kwamba hatuna budi kubadilisha dira, mfumo wetu wa kijamii na kiuchumi, na jinsi tunavyotawaliwa, ikiwa tunataka kuzuia janga kubwa la kutofaulu, lasivyo, tutaendelea kuzama katika lindi la umaskini, unyonge, wasiwasi na migogoro.

4. **NI LAZIMA TUOKE KEKI KUBWA ZAIDI YA KITAIFA** — Wanajopo walibaini kutokana na majadiliano yao na Wakenya kwamba maoni ya kisiasa kuhusu ustawi yanajikita zaidi katika kugawana badala ya kuunda. Hali ya kutowiana kwa uchumi wetu wa kitaifa na matamanio ya kibinafsi na ya pamoja ya kujistawisha ni hatari. Jambo moja muhimu zaidi ambalo Serikali yoyote inaweza kufanyia Wakenya ni kuwapa nguvu na uwezo kwa kujenga uchumi uliokwezwa na uundaji wa thamani.

5. **WAKENYA HAWAWAJALI WALEMAVU**— Wengi wetu hatuzingatii ulemavu kama kitu ambacho sisi wenyewe tunaweza kukumbwa nacho au kinaweza kuathiri mtu anayetutegemea. Tunahitaji, kwa dharura, kutangamana vyema na watu wenye ulemavu ili waishi kama wanajamii kamili wenye haki na fursa sawa kama ilivyo sawa kimaadili, na kama inavyohakikishwa na Katiba.

6. **UKOSEFU WA HAKI KWA VISA VINGI VYA DHULUMA**— Tumechukua mfumo wa kutotendea haki watu wanaodhulumiwa. Kila mwaka, Wakenya wanapitia mateso ya kila aina na dhuluma, ikiwemo wakati wanapotekeleza haki yao ya kisiasa ya kupiga kura. Wao hutafuta haki. Tume huundwa na kuandika ripoti ambazo zinakaa kwenye rafu, pasi na kutekelezwa. Jopokazi linapendekeza kwamba utekelezwaji wa mapendekezo ya ripoti hii, ambayo mengi yana athari kubwa, yanapaswa kujumuisha masilahi na mahitaji ya wahasiriwa wa dhuluma za kihistoria, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa tume zinazotajwa katika kifungu cha 15 zinatekeleza majukumu yazo kuhusu dhuluma za kihistoria ipasavyo.

# Sura ya 2 — Maadili ya Kitaifa

Tunakosa imani, maadili na matamanio ya pamoja kuhusu nini Kenya inaweza kuwa ikiwa sote tutazingatia maadili ya kitaifa ambayo hujenga na kuimarisha umoja wetu. Utaratibu huu ni fursa ya kihistoria kwetu kuanza, kwa hiari, kufafanua, kuendeleza na kuyaambata maono ya pamoja ambayo yataleta umoja Kenya na uwezo wa kukabili changamoto zake zote kuu.Hii ni kazi ya ujima, inayoanzia katika familia na jamii, ikisaidiwa na mikakati inayokumbatia tamaduni nzuri, imani na maadili ya jamii mbalimbali za Kenya na kuwezeshwa na mashirika ya kijamii, sekta ya kibinafsi, na asasi za Serikali. Itajumuishwa katika mfumo rasmi wa elimu, kuanzia chekechea na kudumu milele, asasi za dini na utamaduni, vyombo vya habari, na sekta yetu ya sanaa. Hayatakuwa maadili ya jamii moja bali ya jamii zenye sauti tofautitofauti zilizomotishwa na hamu ya kuchangia, kumiliki na kujenga taifa ambalo ni nyumbani kwetu sote. Hapa chini ni baadhi ya mapendekezo muhimu zaidi ambayo wanajopo wanaamini yatasaidia kujenga maadili thabiti ya kitaifa.

1. **Kazi muhimu zaidi ya kitaifa ni kuwazia mambo makubwa na ya kudumu**— Uchaguzi huja na kuenda na tawala mbalimbali, lakini Kenya itaendelea kuwepo. Tunahitaji maono kuhusu Kenya tunayotaka kuishi katika vizazi vitatu vijavyo au miaka 100. Maono yaliyofumbatwa katika michakato ambayo inaruhusu Wakenya kuyaendeleza zaidi ya chaguzi zinazokuja na kuenda.

2. **Tunapaswa kujipatia historia halisi, inayobadilika, jumuishi na rasmi**. Rais Uhuru Kenyatta anapaswa kuagiza **Historia rasmi ya Kenya** inayorejelea miaka 1000 nyuma na inayotoa maelezo sahihi na halisi kuhusu makazi ya Kenya na wakazi wa sasa; historia zao, historia za uchumi na turathi za makabila yote nchini Kenya; majukumu ya wanawake kihistoria; maelezo kuhusu biashara ya kimataifa ya watumwa na ukoloni; mapambano dhidi ya wakoloni; historia ya kipindi cha baada ya ukoloni katika kila sehemu ya nchi; na historia ya kisasa ikiwemo ile ya maeneo ya mijini na jamii mpya nchini Kenya.

3. **Ni lazima tufurahie ngozi yetu ya Kiafrika**— Jopokazi linapendekeza kwamba Serikali ifanye mipango ya kuoanisha utambulisho wa kisasa wa Wakenya na tamaduni zetu tofauti za Kiafrika ili sisi Waafrika tujisikie vizuri kwenye ngozi yetu na pasiwe na mpaka kati ya hali hizi mbili, au zaidi, wakati mwingine hali kinzani.

   i. Imarisha Wizara ya Utamaduni na Turathi ambayo kwa sasa inaendeshwa na serikali kama shughuli tu ya pembeni.

   ii. Badilisha Siku ya Kufungua Zawadi inayoadhimishwa tarehe 26 Desemba iwe Siku ya Utamaduni Wa Kitaifa kwa kusherehekea utamaduni na kujifunza kuhusu tamaduni zingine za Wakenya (hii inaweza pia kufanywa Januari 1).

   iii. Kukuza heshima ya wazee.

4. **Sisi sote tuna wajibu** — Ni sharti kila sekta kuu ya nchi itekeleze jukumu na wajibu wake kwa umakini zaidi katika kujenga maadili ya kitaifa kutokana na tamaduni tofauti za nchi, masilahi na makundi.

5. **Kukuza maadili wakati wote** — EACC inapaswa kulenga kukomesha uhalifu wa kiuchumi, na majukumu yake ya maadili yasambaziwe NCIC ambayo kuanzia sasa itabadilishwa jina na kuitwa Tume ya Maadili na majukumu yake yaboreshwe sambamba na mwito wa Tume hiyo, na kwamba iwe chini ya Ofisi ya Rais. Pia:

   i. Kufundisha watoto jinsi ya kutoa huduma na kuwajibika kwa kuanzisha Mtandao wa Kujitolea wa Kitaifa unaounganisha vijana na fursa za kujitolea.

   ii. Kufundisha maadili kama somo la lazima katika mtaala wote wa masomo kutoka nasari hadi chuo kikuu.

iii. Kujumuisha mafunzo ya maadili na kanuni za kitaifa kama sehemu ya utamaduni wa kila kabila na hususan kama sehemu ya mafunzo wakati wa sherehe za kuingia utu uzima.

iv. Kutekeleza utaratibu wa sasa wa utekelezwaji sheria chini ya Kifungu kuhusu Uongozi na Uadilifu.

6. **Unganisha amali za kitamaduni na kaida za kisasa** za Wakenya kama inavyoonyeshwa katika sherehe za kitamaduni za kuingia utuuzima na maadili na kanuni za Katiba, na Majukumu na Haki za uraia.

# Sura ya 3 — Majukumu na Haki za Uraia

Tumeweka mkazo sana juu ya kile ambacho taifa linaweza kufanyia kila mmoja wetu - haki zetu - na kusahau kile ambacho kila mmoja wetu anapaswa kufanyia taifa letu. Yafuatayo ni mapendekezo muhimu yaliyotolewa na Jopokazi:

1. Wakenya wana haki kutoka kwa Mungu ambazo sasa ni lazima ziende sambamba na Mkataba wa Majukumu ya Wananchi ambayo yamehamasishwa na Wimbo wa Kitaifa na Maadili ya Kitaifa, na inajumuisha Ahadi ya Uzalendo kwa Taifa na Katiba ya Kenya (kwa shule, mahali pa kazi na katika hafla rasmi za kitaifa na umma).

2. Kuanzisha na kuendesha mipango ya kuendeleza na kusambaza elimu ya uraia kuhusu haki na majukumu.

3. Fundisha watoto utamaduni wa uwajibikaji kwa kubuni mipango ya utendaji na kujitolea shuleni ili kusaidia jamii na asasi zilizo karibu na shule.

4. Kuwatiisha Mawaziri wote na Makatibu Wakuu kwa taasisi za umma wanazoendesha. Ikiwa asasi za umma haziwafai, basi wao hawawafai Wakenya.

5. Kubuni mtaala wa kulea watoto na kufundisha ulezi katika asasi za kidini, vituo vya afya na katika asasi nyinginezo za kijamii, serikali na kitamaduni.

6. Kuhimiza vijana Wakenya kati ya miaka 18 hadi 26 kujitolea kwa kipindi cha miezi sita ya maisha yao kuwatumikia Wakenya kwa hiari.

# Sura ya 4 — Uhasama wa Kikabila na Ushindani

Haya ndio matishio makuu kwa ufanisi wa Kenya na ustawi wa nchi yetu. Jopokazi linapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe:

1. Kuelimisha Wakenya kuhusu tamaduni na mila zao tofautitofauti na kuunda mtaala wa shule unaofundisha wanafunzi kuhusu tamaduni na mila za kila jamii na dini nchini Kenya. Pia, ni sharti shule zote za sekondari za bweni za umma ziandikishe asilimia 50 ya idadi ya wanafunzi wake kutoka nje ya kaunti.

2. **Ondoa mtindo wa urais** wa "mshindi ndiye anayechukua kila kitu", badala yake anzisha mfumo jumuishi wa kisiasa. Hii itabadilisha mfumo wetu wa kisiasa ili uambatane zaidi na desturi za makubaliano ya watu wetu, na kupunguza makali ya kikabila ambayo ndio msingi wa ushindani wa kisiasa anaovuruga ubora wa uchaguzi.

3. Kama njia ya kuunganisha jamii zetu zilizo mipakani, na kubadilisha mfumo wetu wa sasa wa kisiasa na kikabila, huku tukijenga uchumi uliostawi zaidi, **tuharakishe mchakato wa Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki** kama hatua ya kuafikia Shirikisho la Kisiasa.

4. **Hakikisha kwamba usambazaji wa rasilimali haufanywi kwa usawa pekee bali pawe hasa na hisia za usawa** - Punguza migogoro kuhusiana na usambazaji wa rasilimali za kitaifa kwa kuwachukulia Wakenya wote kuwa sawa - hii inapaswa kuzingatia idadi ya watu, uwekezaji unaohitajika katika sekta za afya na kilimo, utoaji wa huduma, na upatikanaji wa rasilimali asili na fursa za kuishi

5. **Baraza la washauri** — Kwamba Rais kama Nembo ya Umoja wa Kitaifa anapaswa kuwa na ushauri wa kibinafsi wa watu mashuhuri, wenye uzoefu, na wenye heshima wanaohudumu katika Baraza la Washauri pasi na kulipwa mishahara.

6. **Imarisha ofisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa** ili kuiwezesha kushughulikia tatizo la ubaguzi wa kisiasa kwa kuajiri na kuteua Msajili ambaye ni huru, anayejiamini na mchapa kazi.

# Sura ya 5 — Chaguzi zenye kuleta Migawanyiko

Jopokazi linapendekeza mfumo ambao utashughulikia mahitaji yetu ya kipekee, hususan katika kuunda mfumo wa ndani ya nchi au wa kiasili utakaolainisha mamlaka makuu ya nchi na uwakilishi.

1. **Muundo wa mamlaka makuu asilia ya kitaifa** - Kuwasikiliza Wakenya kote nchini na kusikia maoni yao kunadhihirisha kuwa wanataka mfumo wa kiasili ambao unaonyesha ujumuishaji katika Mamlaka Makuu, na wakati huohuo wakiwa wanataka kumchagua Rais wao moja kwa moja. Pia waliwaambia Wanajopo kwamba wanataka upinzani wenye mamlaka na Bunge ambalo litawawajibisha wenye Mamlaka Makuu.

Muundo wa aina hii una sifa zifuatazo:

i. **Kugombea na kushinda Urais -** Rais atachaguliwa kupitia haki ya kimsingi ya raia kupiga kura. Ili mgombeaji atangazwe mshindi wa Uchaguzi wa Rais, anapaswa kushinda asilimia 50 + 1 ya kura za Urais na angalau asilimia 25 ya kura zilizopigwa katika kila ya zaidi ya nusu ya Kaunti zote, kama ilivyo sasa.

ii. **Rais mwenye Mamlaka** — Rais atasalia kuwa Kiongozi wa Nchi na Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Yeye atakuwa nembo kuu ya Umoja wa Kitaifa. Rais atakuwa mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri, ambalo linajumuisha Naibu Rais, Waziri Mkuu, na Mawaziri.

iii. Kitengo cha Utawala, kwa ruhusa ya Rais, kitakuwa na uwezo wa kuamua sera ya Serikali kwa ujumla, huku Mawaziri, chini ya uongozi wa Waziri Mkuu, watawajibika katika Bunge la Kitaifa kutekeleza shughuli za serikali kwa pamoja.

iv. **Mihula ya Utawala** - Dumisha mihula miwili ya sasa ya utawala kwa cheo cha Urais.

v. **Naibu Rais** - Naibu Rais ndiye mgombeaji mwenza wa Rais. Yeye ndiye atakayekuwa naibu wa Rais.

vi. **Waziri Mkuu**— Katika muda wa siku maalum zilizowekwa kufuatia kuitishwa kwa Bunge baada ya uchaguzi, Rais atamteua Waziri Mkuu, ambaye atakuwa Mjumbe wa Bunge la Kitaifa aliyechaguliwa kutoka kwa chama cha kisiasa chenye idadi kubwa zaidi ya wabunge katika Bunge la Kitaifa au, ikiwa hakuna chama cha kisiasa chenye wabunge wengi, atateuliwa yule aliye na uungwaji mkono kutoka kwa idadi kubwa ya wabunge.

vii. **Kuidhinishwa na Bunge** — Aliyeteuliwa kwa cheo cha Waziri Mkuu hatachukua mamlaka hadi kwanza uteuzi wake uthibitishwe na azimio la Bunge la Kitaifa linaloungwa mkono na idadi kubwa ya Wabunge.

viii. Ikiwa uteuzi wa Waziri Mkuu hautathibitishwa, Rais atachukua idadi fulani ya siku za kuteua mwingine. Utaratibu huu utaendelea hadi pawe na uteuzi wa Waziri Mkuu utakaothibitishwa. Hatua ya kuhakikisha kuwa mchakato huu sio wa kudumu, na kwamba utawala unaendelea unapaswa kuzingatiwa. Jopokazi lingependa pia kusema kwamba baadhi ya raia walionyesha wasiwasi kwamba kukosa idadi kubwa ya wabunge wanaounga mkono uteuzi wa wadhifa huo kunaweza kulemaza ushirikishi katika siasa za Kenya. Kulikuwa na mapendekezo ya kuongeza kiwango na kuhitaji idadi kubwa ya uungwaji mkono. Jopokazi lilihisi kwamba suala hili lilihitaji majadiliano mapana ya kitaifa.

ix. **Kufutwa kazi**— Waziri Mkuu anaweza kufutwa kazi na Rais au kupitia kura ya kutokuwa na imani naye katika Bunge la Kitaifa.

x. **Kiongozi Rasmi wa Upinzani**— Mwaniaji atakayeibuka wa pili katika uchaguzi wa Urais anakuwa Mbunge ambaye hajachaguliwa na Kiongozi Rasmi wa Upinzani iwapo chama chake hakijawakilishwa katika Serikali, au muungano wa vyama vya Bunge ambavyo havijawakilishwa katika Serikali.

xi. **Hitaji la kuwa na upinzani wenye nguvu** — Chama au muungano wa vyama visivyowakilishwa Serikalini vitakuwa Upinzani Rasmi.

xii. **Baraza la Mawaziri la Upinzani** — Kiongozi Rasmi wa Upinzani atawezeshwa kuteua Baraza la Mawaziri watakaopiga msasa utendakazi wa Serikali katika Bunge. Hii itahusisha uwezo wa kuwa na utafiti bora kuhusu sera na ajenda ya sheria za Serikali.

xiii. **Kipindi cha Maswali** — Upinzani utakuwa na jukumu muhimu katika Vikao vya Waziri Mkuu na Mawaziri wakati wa Maswali Bungeni. Kipindi hicho cha Maswali ni fursa kwa Wabunge kuuliza Mawaziri wa Serikali maswali kuhusiana na mambo wanayowajibikia.

2. **Majukumu ya Waziri Mkuu** —

xiv. Waziri Mkuu atakuwa na mamlaka juu ya usimamizi na utekelezwaji wa majukumu na shughuli za kila siku za Serikali.

xv. Waziri Mkuu atakuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Bunge la Kitaifa.

xvi. Waziri Mkuu atajukumiwa na Rais kusimamia kamati ndogo za Baraza la Mawaziri.

xvii. Katika utumiaji wa mamlaka yake, Waziri Mkuu atafanya au ataelekezwa kufanya jambo au mambo yoyote ambayo Rais ameagiza yafanywe.

xviii. Waziri Mkuu ataendelea kupata mshahara wake kama Mbunge bila ya mshahara wa ziada kwa majukumu ya uwaziri mkuu.

xix. Katibu wa Kudumu/Katibu asiye wa kudumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu atasimamia Kamati ya Utekelezaji ya Kiufundi ya Makatibu wa Kudumu/Wasio wa Kudumu.

xx. Ili kuondoa siasa katika Utumishi wa Umma, Makatibu Wa Kudumu au Wasio wa kudumu hawataidhinishwa na Bunge. Wajibu wao utakuwa wa kiutawala na kiufundi pekee.

3. **Baraza mseto la mawaziri** — Baraza la mawaziri ni sehemu muhimu ya Kitengo cha Utawala wa Serikali. Ukitathmini maoni ambayo Wanajopo walipokea kutoka kwa Wakenya, kuna hali ya kutoridhika na mfumo wa sasa wa baraza hilo. Jopokazi linapendekeza utaratibu ufuatao katika kuunda Baraza la Mawaziri:

xxi. Rais atateua Mawaziri baada ya kushauriana na Waziri Mkuu. Mawaziri watawajibikia ofisi ambazo Rais atabuni kulingana na Katiba.

xxii. Baraza la Mawaziri litajumuisha wabunge na wataalamu, watalaamu watafanywa kuwa wabunge ambao hawajachaguliwa baada ya kuidhinishwa na Bunge.

xxiii. Jopokazi pia linapendekeza Waziri aitwe 'Cabinet Minister' badala ya 'Cabinet Secretary'.

xxiv. Ili kuhakikisha kuwa pana mwelekeo mzuri zaidi wa kisiasa na uwajibikaji katika Bunge, kutakuwa na nafasi ya Waziri wa Serikali atakayeteuliwa na wabunge wa Bunge la Kitaifa na kuchukua mwelekeo katika majukumu yao ya uwaziri kutoka kwa Mawaziri. Mawaziri hawa wa Serikali wataendelea kupata mshahara wao kama wabunge bila ya mshahara wa ziada kwa majukumu yao ya uwaziri.

## 4. Uwakilishaji

**Uwakilishaji katika mfumo wa uchaguzi** — Ni muhimu kwamba bila kujali mkondo utakaochukuliwa na mageuzi ya uwakilishaji, yanapaswa kufuata kanuni zifuatazo ikiwa Wakenya watawakilishwa kwa usawa:

xxv. Kwamba chaguo la watu, kama inavyoonyeshwa katika uchaguzi wa wawakilishi wao, zikiwemo chaguzi ndogo za Vyama na teuzi, litapitishwa kupitia uchaguzi wa haki, huru na wazi.

xxvi. Watu waliojumuishwa katika orodha yoyote ya Chama watakuwa tayari wamehusishwa kwenye mchakato wa kushiriki mazungumzo ya wazi ya umma katika Kaunti hata kabla ya utaratibu mwingine wowote wa kuwapiga msasa.

xxvii. Kwamba kutakuwa na usawazishaji katika uwakilishi na usawa wa uraia kadiri iwezekanavyo, kwa kuhakikisha kwamba kila kura ya Mkenya inayo hadhi na nguvu, kama inavyotajwa katika Katiba.

xxviii. Kupitia kwa Sheria ya Vyama vya Kisiasa, vyama vitalazimishwa kufuata Katiba ili kuafiki Sheria ya Jinsia na sheria nyingine za Katiba zinazohusu ushirikishwaji kupitia orodha ya vyama vyao. Hii itasawazisha jinsia zote mbili katika mahusiko ya

kisiasa, badala ya kuunda mfumo sambamba ambao hujenga dhana ya ushirikishi tu.

xxix. Orodha ya Madiwani wa chama itafuata kanuni na michakato sawa ya ushiriki wa mijadala ya umma, uchaguzi na kuwapiga msasa kama ilivyo katika Bunge la Kitaifa. Hii itahakikisha kwamba kuna uwajibikaji wa moja kwa moja miongoni mwa watu na vyama.

xxx. Maeneobunge yote 290 ya sasa yatahifadhiwa, vikiwemo viti vilivyolindwa kwa sababu vimekuwa vya uwakilishi muhimu wa maeneo ya idadi ndogo ya watu.

xxxi. Gatua vyama vya siasa ili viwe na matawi imara katika Kaunti na ili viruhusu watu kuwa na vikao vya kisiasa na njia za kuwafanya viongozi waliowachagua wawajibike katika muhula mzima wa uongozi, sio tu wakati wa uchaguzi.

xxxii. Orodha za uteuzi kupitia kwa vyama zinapaswa kukamilishwa kwa utaratibu wa uwazi unaosimamiwa na vyama vya siasa na kukaguliwa na Msajili wa Vyama vya Kisiasa na IEBC.

Kuna pia mapendekezo ya Jopokazi kuhusu mabadiliko kwa **Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka**. Hii ni pamoja na:

i. Pawe na Utaratibu utakaowapa viongozi wa vyama vya kisiasa bungeni jukumu la kuajiri Makamishna wa IEBC. Katika kufanya uteuzi wa Makamishna, viongozi wa vyama vya kisiasa wanapaswa kuteua watu wasioegemea kokote, walio na rekodi ya ustadi na uadilifu, na wasiojulikana kuwa wafuasi wa kisiasa au wanaharakati wa chama hicho.

ii. Kulingana na maoni ambayo Jopokazi lilipokea kutoka kwa Wakenya, imani katika IEBC ingali chini. Kwa hivyo, Jopokazi linapendekeza kwamba pawe na mwanzo mpya tunapoelekea

kwenye uchaguzi ujao ili kuimarisha imani ya Wakenya katika taasisi hiyo.

iii. Wafanyikazi wote wa IEBC wanapaswa kuajiriwa kwa kandarasi ya miaka mitatu, wanaweza kusaini upya kandarasi nyingine mara moja pekee, ikiwa utendakazi wao ni mzuri. Vinginevyo, itakuwa imetamatika. Hii itazuia kuendeleza makosa kwa kuwezesha kila Tume ifanye uteuzi wakati mmoja katika muhula wake.

iv. Maafisa wanaosimamia uchaguzi wanapaswa kuajiriwa kupitia mchakato kama ule unaotumika kuajiri makamishna, ikiwemo kushiriki katika mijadala ya umma. Mwishoni mwa mchakato wa kuajiri maafisa wa kusimamia uchaguzi, IEBC inapaswa kupokea ripoti kuhusu uamuzi waliofanya na sababu zilizowapelekea kufanya uamuzi huo. Hili linapaswa kuwekwa wazi kwa umma.

v. Maafisa wanaosimamia uchaguzi wanapaswa kuwa wakandarasi wa muda na haifai kusimamia uchaguzi mkuu zaidi ya mmoja.

vi. Mtu yeyote aliye na uzoefu wa usimamizi wa angalau miaka kumi na mitano (15) katika kiwango cha juu anapaswa kufuzu kuomba nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa IEBC. Wadhifa huo haupaswi kutengewa mawakili pekee. Hata hivyo, mmoja wa Makamishna anapaswa kuwa wakili.

vii. Maafisa wakuu wote wa sasa wa IEBC wanapaswa kupigwa msasa.

viii. Bainisha majukumu ya Katibu na Afisa Mkuu Mtendaji; mfanye Mwenyekiti wa Tume kuwa Afisa Mkuu Mtendaji.

ix. Muundo wa Tume lazima uonyeshe Uso wa Kenya katika viwango vyote.

x. Tafiti njia za kutunga vifungu ambavyo vitapunguza gharama kubwa za uchaguzi wetu. Mfumo wa kuunda orodha za vyama ni mojawapo.

xi. Fanyia mageuzi mfumo wa sasa wa uchaguzi ili kuhakikisha kuwa ni rahisi, sahihi, wenye kuthibitishwa, salama, ulio na uwajibikaji na wazi kama inavyosisitizwa katika Kifungu cha 86 cha Katiba.

# Sura ya 6 — Ushirikishwaji

Jopokazi linatoa mapendekezo makuu katika kuimarisha ushirikishwaji kwa misingi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kidini, kitamaduni, vijana, na kijinsia. Hapa kuna baadhi yake:

1. **Mwandishi Maalum wa Masuala ya Ushiriki wa Umma**— Kuimarisha ubora, uwazi, na ushirikishwaji katika michakato ya ushiriki wa umma unaohitajika Kikatiba kwa kubuni Ofisi ya Mwandishi Maalum wa kushughulikia Ushiriki wa Umma. Ofisi hiyo itapewa jukumu la kuandaa shughuli za kuushirikisha umma kwa niaba ya taasisi zote za serikali na zisizo za serikali zinazotekeleza mipango ya sera na utendaji ambayo, Kikatiba, inahitaji ushiriki wa umma. Mwandishi Maalum wa Masuala ya Ushiriki wa Umma anapaswa kuweka rekodi sahihi kuhusu ushiriki wa umma hadharani na aweze kukidhi haja za asasi zinazotaka huduma yake. Kando na jukumu la kuimarisha uwazi na kufanikisha ushiriki wa umma, ongezea ofisi hiyo jukumu ambalo litasababisha ubishi kuhusu maslahi ya umma kwa namna ambavyo inakingwa dhidi ya ushawishi wa msambazaji/mchuuzi. Mfano wa jinsi jambo hili linaweza kufanya kazi katika mfumo wa demokrasia unapatikana katika kielelezo cha India.

2. **Jamii zilizotengwa hazifai kuwatenga wengine**— Ithibati kutokana na mashauriano ya BBI katika kaunti inaonyesha maoni yenye uzito kwamba baadhi ya jamii ambazo zililalamika kuhusu kutengwa katika ngazi ya kitaifa zenyewe zilikuwa na hatia ya kutenga jamii za watu wachache katika Kaunti husika. Kwa hivyo ilikuwa wazi kuwa mageuzi ya kukuza ushirikishwaji katika ngazi ya kitaifa yanapaswa pia kuonekana katika kiwango cha Kaunti.

3. **Uraia wa mataifa mawili -** Kuhusu suala la Wakenya walio na uraia wa mataifa mawili kuwa wasioaminika kwa msingi huo, huo unakuwa

ubaguzi na kiwango ulinzi na utambulisho wao unarudi chini. Wakenya walio tayari kuwa watumishi wanapaswa kupimwa kwa vigezo vya tabia na utendakazi wao mzuri na si kudhaniwa kuwa wamegawa uaminifu wao kuwili, ambao unatia doa maadili na uzalendo wao. Kwa hivyo, mipaka ya uwezo wa raia wa mataifa mawili kuwahudumia Wakenya unapaswa kuwa mdogo zaidi. Mfano mmoja ni kuhusu vikosi vya ulinzi, ambavyo kikatiba vinaweza kuamrishwa kushambulia wanajeshi wa nchi nyingine ambazo vikosi hivi vinaweza kuwa na uraia nazo. Kwa kuzingatia uchunguzi huu, Jopokazi linapendekeza kwamba watumishi pekee wa Serikali wanaoweza kuwekewa mipaka ya kuwa na uraia wa mataifa mawili wawe Amiri Jeshi Mkuu wa Kikosi cha Ulinzi, wanachama wa vikosi vya ulinzi, na uanachama wa Baraza la Ulinzi.

# Sura ya 7 — Ustawi kwa Wote

Tunahitaji mapinduzi ya kiuchumi, ili kujenga uchumi ambao unaweza kuzalisha kazi tunazohitaji, haraka. Wakenya walioongea katika kila kikao cha mashauriano kinachoendeshwa na Jopokazi, katika kila Kaunti, walizungumzia matatizo yao yanayochangiwa na umaskini na ukosefu wa kazi au ajira za mapato duni. Changamoto moja muhimu inayokabili Wakenya kuhusu suala la ustawi wa pamoja ni kuunda kazi za kutosha na ajira, haswa kwa vijana. Haitoshi tu kuboresha uchumi wetu na kupanua uwekezaji: ni lazima tuibadilishe kabisa mfumo wa uendeshaji wa uchumi wetu ikiwa tunataka kukabiliana na ukosefu wa kazi uliopo sasa. Baadhi ya Mapendekezo machache makuu katika ripoti ni:

1. **Mkakati wa miaka 50 —** Tunahitaji kupanua mawazo yetu yawe ya kudumu ikiwa tunataka kujenga uchumi ambao unakidhi mahitaji ya vizazi vya sasa na vijavyo. Anza na mkakati wa miaka 50 ambao lengo lake kuu ni kuifanya Kenya iwe miongoni mwa mataifa bora zaidi ulimwenguni kwa chumi zilizostawi, za pamoja na endelevu.

2. **Kujenga masoko kana kwamba ni bidhaa za umma —** Serikali inapaswa kuwa katika harakati za kuendelea kujenga masoko na kuyapanua masoko hayo kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na nguvu kazi ya Wakenya katika mataifa jirani kupitia utangamano zaidi.

3. **Kutoa mikopo kwa sekta muhimu —** Serikali inapaswa kubuni sera inayotoa miongozo ya kisheria na kiudhibiti kwa benki ili ziweze kutoa mikopo kwa sekta muhimu kama za biashara ndogo ndogo, uuzaji bidhaa nje ya nchi, uzalishaji, makazi, elimu, afya, nishati mbadala, usafi wa mazingira na utupaji wa taka, na kilimo (ikiwemo mifugo na uvuvi).

4. **Ustawi wa viwanda unahitaji kuwa lengo kuu la Serikali –** Ni ustawi wa viwanda pekee unaoweza kukuza vipaji vya Wakenya na ni ndoto ya kuendeleza ustawi wa taifa. Ni muhimu kwa Wakenya na Serikali kujitenga na gumzo linaloshamiri kwamba Kenya na mataifa ya Afrika hayawezi kujistawisha kiviwanda kwa sababu ya kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia, kwa mfano katika matumizi ya roboti.

5. **Kulinda uvumbuzi wa Wakenya, rasilimali za kinasaba, maarifa ya jadi na misemo kama aina ya mali iliyolindwa kisheria -** Mustakabali wa uchumi wa dunia uko katika ubunaji na uvumbuzi kwa kutumia utaalamu wa kiakili, uundaji ramani na matumizi ya msimbo wa kinasaba, na hazina hai ya maarifa ambayo imeandaliwa na vizazi vya jamii zetu.

6. **Akiba ni uwekezaji —** Fanya juhudi kubwa ya kuongeza akiba ya kitaifa kwa angalau asilimia 25 ya Pato la Taifa ikiwa Kenya inataka kuendeleza uwezo wake wa kuimarisha uwekezaji katika sekta mbalimbali, kikiwemo kituo cha nguvu kazi madhubuti cha uzalishaji ili kuunda nafasi za kutosha za kazi kwa Wakenya

7. **Mapato kutoka kwa Wakenya waishio ng'ambo--** Usitegemee pesa kutoka ng'ambo pekee bali toa vivutio, kinga na taratibu za kuruhusu Wakenya wanaoishi ng'ambo kuweka zaidi akiba zao nchini Kenya.

8. **Tumia pesa kwa maendeleo, si kwa urasimu pekee -** Tumia pesa nyingi kwenye maendeleo kama sehemu ya mapato ya serikali ili kuongeza bidhaa za umma na huduma kwa Wakenya. Lenga uwiano au kikomo cha juu, ulioandikwa kuwa sheria, wa angalau 70:30 kwa maendeleo dhidi ya matumizi ya kawaida.

9. **SRC na mishahara—** Ni sharti kuwe na ufafanuzi kuhusu mamlaka ya kisheria na kiutawala ya Tume ya Mishahara na Marupurupu ili kuhakikisha kuwa inasimamia masuala yote yanayohusiana na nyongeza za mishahara.

10. **Ushuru —** Ijapokuwa mawanda ya ushuru yanahitaji kupanuliwa ni muhimu kwamba utozaji wa jumla wa ushuru nchini Kenya uwe chini kiasi kwa chumi shindani za kieneo na kimataifa. Wazia mbinu mpya za kurahisisha utozaji ushuru, ikiwemo fikra ya kuanzisha kiwango Sawa cha Ushuru kwa mapato ya juu kuliko ya Mshahara Unaokidhi Mahitaji ya Kimsingi.

11. **Lenga wakulima, wafugaji na wavuvi —** Lipe kipaumbele suala la kumaliza ufisadi miongoni mwa wanaotekeleza miradi ya kilimo na

ufugaji katika juhudi za kupambana na uovu huo. Imarisha viwanda vya mashambani kama msingi wa kuendeleza aina za kisasa zaidi za uzalishaji.

12. **Kuimarisha Kifungu 43 cha Katiba kuhusu haki za kiuchumi na kijamii**
    i. Serikali ya Kitaifa na Serikali za Kaunti zinapaswa kubuni sera na kanuni za kuongoza utekelezwaji kwa uangalifu wa Kifungu cha 43 cha Haki za Kiuchumi na Kijamii.

    ii. **Manifesto za vyama** -- Kifungu 43 cha Haki za Kiuchumi na Kijamii kinapaswa kutekelezwa kwa uangalifu na viongozi wote waliochaguliwa na manifesto zote za uchaguzi za vyama vyao vya kisiasa. Hii itahitaji Vyama vyote vya Siasa kuunda maono na sera za utekelezwaji wa Mswada wa Haki (unaojumuisha Haki za Kiuchumi na Kijamii) kama sehemu ya manifesto zao za kampeni za uchaguzi.

13. **Hakuna Mkenya ataachwa nje —'Mpango wa Kubadili'**: Kama sehemu ya kuhakikisha kwamba Wakenya wote wanapata huduma bora ambazo ndio msingi wa kuwaweka watu kwenye njia ya ustawi wa pamoja, Jopokazi linapendekeza 'Mpango wa Kubadili' ili kuyavuta maeneo yaliyotengwa hadi kwenye kiwango bora kinachostahiwa maeneo mengine.
14. **Tumia rasilimali chache za umma kwa maendeleo, si kwa urasimu pekee** — Tumia pesa nyingi kwa maendeleo kama sehemu ya mapato ya serikali ili kuongeza bidhaa za umma na huduma kwa Wakenya. Lenga uwiano au kikomo cha juu, ulioandikwa kuwa sheria, wa angalau 70:30 kwa maendeleo dhidi ya matumizi ya kawaida.
15. **Kuza na fungua nafasi kwa vijana ili waonyeshe mipango, ubunifu na ujasiriamali wao**— Kwa kuongeza nafasi za ajira na njia za kupata riziki kwa kufanya biashara ndogo ndogo zishindane kwa urahisi na kukua bila Serikali kuziwekea mazingira magumu na ghali kwao kufanya kazi.

i. Taifa liandae na kuzindua mbinu rahisi za wanabiashara wadogowadogo wa Kenya kufanya biashara na kutotegemea vielelezo vya kufanya biashara vinavyoandaliwa na wageni kwa ulinganishi wa kimataifa. Hii inapaswa kuwa tathmini linganishi ya KNBS ya kila mwaka ambayo haijagawanywa kijiografia - kaunti, majiji na miji - na itangazwe.

ii. **Punguza kutoza biashara ndogondogo na mpya ushuru** kwa kuwapunguzia ushuru kwa angalau miaka saba kama njia ya kuinua ujasiriamali wa vijana na uundaji wa nafasi za kazi.

iii. **Ubunifu na michezo** — Fanya juhudi za kimakusudi za kuratibu, kuhamasisha na kukuza ubunifu na michezo, miongoni mwa sekta nyingine ambazo vijana wa Kenya huonyesha uwezo mkubwa na ari.

iv. Himiza Sekta ya Kibinafsi kuunda wakfu wa kitaifa, usio wa biashara ambao utasimamiwa na Rais na ambao utatumiwa kutoa ushauri, mafunzo, na zana za kuwasaidia vijana wa miaka 18-35 wanaopania kuwa wafanyabiashara.

v. Ili kuwasaidia vijana kuanzisha biashara, fungua meza ya ushauri katika kila Kituo cha Huduma Centre kinachosimamiwa na mtaalamu wa maendeleo ya kibiashara.

vi. **Kujiajiri na Elimu ya kiufundi** — Ni muhimu tuondoe dhana kwamba kazi ya ufundi ni ya wale ambao wameshindwa katika masomo kwa kuunda njia mbili sawa kati ya mafunzo ya kitaaluma na ya ufundi.

# Sura ya 8 — Ufisadi

Dhana iliyokita mizizi miongoni mwa Wakenya kwamba kuwa na serikali inayotawala kiharamu huwatuza wandani wake nyadhifa serikalini na kuendeleza ufisadi, kinyume na utendakazi bora na bidii, ndilo tishio kuu kwa utangamano na usalama. Jopokazi linatoa mapendekezo makuu na yenye kutekelezeka, baadhi yake yametajwa hapa chini.

1. Komboa Kenya kutokana na wakiritimba kupitia mikakati ya kuvunja miungano wa wakiritimba na kuwaadhibu wahusika ipasavyo.
2. Kuhimiza ufichuaji wa ufisadi kwa kuwapa wanaofichua shughuli za ufisadi asilimia 5 ya pesa zilizorejeshwa.
3. Kuwalinda wafichuzi wa ufisadi - Wezesha taratibu za mahakama ambazo zinahakikisha usalama na ulinzi kwa watoaji habari, wafichuzi na mashahidi, hususan kuhusu ugaidi, uhalifu mkubwa wa kimataifa, na ufisadi.
4. Piga marufuku watumishi wote wa umma kufanya biashara na serikali. Pia hawapaswi kujihusisha na biashara nje ya serikali isipokuwa ikiwa shughuli wanazotaka kujihusisha nazo zinaidhinishwa.
5. Fanya fomu zote za kutangaza mali ziwe wazi kwa umma.
6. Fanya Kenya iwe nchi inayotoa huduma kupitia mfumo wa elektroniki kwa asilimia 100 kwa kuweka kidijitali huduma zote za serikali, michakato, mfumo wa ulipaji na uwekaji wa rekodi.
7. Zidisha imani ya raia kwa Idara ya Mahakama kwa kutambua kuwa mihimili mikuu ya katiba nchini Kenya ni kutenganisha mamlaka, kati ya vitengo vikuu vya Serikali, na uwajibikaji kwa Wakenya. Ni sharti uhuru wa Mahakama ulindwe kama mhimili mkuu, lakini nayo pia inapaswa kuwajibikia Wakenya.
8. Ili kuimarisha mchakato wa kuyajibu malalamishi katika mahakama, Ofisi ya Wakili wa Wananchi inahitaji mageuzi ili iweze kufikiwa na umma na kushughulikia haja zao.

9. Linda uhuru wa vyombo vya habari ili kufichua ufisadi lakini hakikisha kuwa madai ya uwongo na kuharibu jina hakutatizi utoaji wa huduma kwa watu.

10. Tumia mbinu ya kuzuia na kukatisha tamaa kwa kuhakikisha kuwa umma umehamasishwa vyema kuhusu maadili kupitia mafunzo na elimu, kuwatuza wafichuzi wa ufisadi na kutathmini utendakazi.

11. Punguza ubadhirifu na uozo katika Mashirika ya Serikali wa kuwa wasimamizi wasiojali wakitarajia dhamana ya Serikali kwa hatua zifuatazo:

    - Kuimarisha uwezo wa Mdhibiti wa Bajeti ili aweze kugundua mapema na kushughulikia kwa wakati unaofaa matumizi mabaya ya pesa, ubadhirifu, na michakato iliyo haramu.
    - Kama Rais alivyoamrisha mnamo Novemba 2015, lainisha mashirika ya umma kwa kujikita zaidi kwenye lengo la kimsingi la shirika husika na kupunguza ubadhirifu wa fedha kwa kutunga Mswada wa Mageuzi ya Mashirika ya Umma.

# Sura ya 9 — Ugatuzi

Kuhusu suala la kuondoka mamlakani baada ya utawala wa nchi na usimamizi wa rasilimali za umma, ugatuzi umekuwa na ufanisi mkubwa. Hata hivyo, ugatuzi bado unazongwa na changamoto tele ambazo ikiwa hazitatafutiwa ufumbuzi, kutaibuka maswali kuhusu uendelevu wake kisiasa na kiuchumi. Mapendekezo makuu yaliyotolewa na Jopokazi ni pamoja na yafuatayo:

1. Dumisha kaunti zote 47 lakini himiza na usaidie kaunti kuunda, kwa hiari, maeneo ya kiuchumi.

2. Ongeza pesa katika kaunti kwa angalau asilima 35 ya akaunti za mwisho zilizofanyiwa mahesabu.

3. Wakati wa kutenga pesa katika kaunti, tumia fomula inayolenga kuhakikisha kwamba huduma zinafikia maeneo ya wakazi halisi ili pesa zisitolewe kwa misingi ya ukubwa wa eneo.

4. Kamilisha uhamishaji wa majukumu kutoka Serikali ya Kitaifa hadi Serikali za Kaunti na ondoa urudiaji wote wa majukumu kati ya ngazi hizo mbili za serikali.

5. Fuata usemi "pesa hufuata majukumu" katika kutenga pesa kati ya ngazi mbili za serikali.

6. Zingatia jinsi Wawakilishi wa Wadi wanavyoweza kusimamia fedha za basari pekee, huku wakihakikisha kuwa hakuna mgongano kati ya matumizi ya fedha za CDF na fedha za kaunti katika maendeleo ya Kaunti.

7. **Mabadiliko katika Usimamizi wa Kaunti** —

    i. Iwapo nafasi ya Naibu Gavana itakuwa wazi kwa sababu zozote zile, kisha Gavana akose kuteua naibu kwa muda wa siku 90, basi Spika wa Bunge la Kaunti atateua Naibu Gavana kwa idhini ya bunge la kaunti.

   ii. Mgombea mwenza wa yule anayewania ugavana hawezi kuwa wa jinsia moja naye. (Gavana akiwa wa kiume, naibu wake ni wa kike).

8. **Tume ya Huduma za Afya** - Hamisha wafanyikazi katika sekta ya afya kutoka serikali za kaunti hadi Tume huru ya Huduma za Afya ili kuweza kugawana wataalamu wa afya walio wachache.

9. Gharama za usimamizi wa Bima ya Kitaifa ya Afya (NHIF) zinapaswa kupunguzwa zaidi kwa kutumia teknolojia, kupunguza visa vya ufisadi na kuongeza tija. Gharama hizi za kiusimamizi zinapaswa kuwa kati ya 5 na 10.

10. Kuandaa na kupitisha mswada wa haki za mgonjwa ili kusawazisha ubora wa huduma za afya katika kaunti zote.

11. **Matumizi ya Pesa katika Serikali za Kaunti -** Usimamizi wa Matumizi ya Pesa katika Kaunti, uwekezaji na utoaji wa nafasi za kazi havifanikiwi katika viwango vingi, hali inayosababisha ubadhirifu mkubwa wa pesa na ufisadi ambao unatatiza ugatuzi. Ufisadi ni janga ambalo ni maarufu sana kwa Wakenya. Ni muhimu pia kwamba uangalizi wa pesa hizo unaimarishwa.

   i. Jibu linapaswa kuwa uangalizi wa pesa ulioimarishwa na mashirika husika, hatua za kupunguza ubadhirifu, na kutenga sehemu kubwa ya fedha za Kaunti kwa maendeleo.

   ii. Kufadhili maendeleo ya kila Wadi kwa hadi asilimia 30 ya bajeti ya maendeleo ya Kaunti katika kipindi cha miaka mitano.

   iii. Uwiano kati ya matumizi ya fedha za maendeleo na matumizi ya kawaida unapaswa kuwiana na ile ya kitaifa kwa 70:30.

   iv. Kuimarisha uhuru wa Mabunge ya Kaunti ya uangalizi wa fedha kwa kuhakikisha kuwa upitishaji na usimamizi wa bajeti za Bunge la Kaunti unalindwa kutokana na kuingiliwa kiholela au kisiasa na Maafisa Wakuu wa Kaunti; michakato hii inapaswa pia kupigwa msasa mkali na usimamizi wa fedha za umma.

v. Hitaji la serikali mpya kukamilisha miradi iliyoanzishwa na magavana wa zamani na Hazina ya Kitaifa kuzuia fedha za miradi mpya hadi ile ya zamani ikamilike. Ni sharti gavana ambaye anataka kuachana na mradi wa zamani awasiliane rasmi na umma akitoa sababu mwafaka za kufanya hivyo.

12. **Kaunti pia zipanue mawanda ya vitega-uchumi** — Kaunti zinapaswa kuongozwa na lengo kuu la kuvutia wakazi wake zaidi katika ujasiriamali, na uwekezaji kutoka sehemu nyinginezo za nchi, na nje ya nchi, uelekezwe kwenye Kaunti.

- Katikati ya haya ni kwamba udhibiti na ukusanyaji wa mapato unaofanywa na Serikali ya Kaunti usivuruge vivutio vya uwekezaji na ubunifu.
- **Biashara mashinani** — Ni lazima kila Kaunti ifanye juhudi kubwa za kimakusudi kusaidia makundi ya wenyeji ili kukuza biashara kupitia ushirika. Serikali ya Kaunti inapaswa kuhakikisha kuwa kuna utaratibu mwepesi wa kuanza biashara ndogondogo na zile zinazoanza, na kwamba ni rahisi kwa wafanyabiashara kufuata kanuni na urasimu, huku bidhaa zao zikifika sokoni kwa wakati unaofaa.
- Kila Kaunti ianzishe na kutangaza Kanuni ya Ujasiriamali na Uwekezaji ambayo itaitumia kwa njia inayotabirika na thabiti.
- Hata ingawa Kaunti zinainua mapato yake, ni lazima zidhibiti ufujaji zikijua fika kwamba zinashindana si tu na Kaunti nyingine nchini lakini pia na nchi nyinginezo na majimbo yazo.

13. **Hakuna kutoza ushuru mara mbili na pia hakuna sheria mbili za ushuru katika ngazi ya Kitaifa na Kaunti** — Taratibu za serikali na serikali nyingine zinapaswa kuundwa na kubainishwa ili kuhakikisha kuwa lengo hili linatimizwa kila wakati.

14. **Kaunti zenye utangamano zaidi** — Kuimarisha mazungumzo na mshikamano wa kijamii katika Kaunti, hususan kaunti ambazo zina

makabila mengi, kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii zenye idadi ndogo ya watu zinasikika na kuheshimiwa.

# Sura ya 10 — Usalama na Ulinzi

Wakenya waliambia Wanajopo kwamba hawajisikii salama. Jopokazi lilibaini kwamba Kenya iko katika eneo hatari na vitisho vya ugaidi vinavyozidi kujitokeza, mataifa yenye utawala unaoyumba au dhaifu na nchi zenye mizozo ya kimipaka, unyanyasaji wa polisi na matendo haramu ya kijambazi yanayokiuka haki za binadamu. Jopokazi linapendekeza hatua madhubuti zifuatazo:

1. **Sawazisha thamani ya maisha ya Mkenya katika kila sehemu ya nchi -**Thamani ya maisha iliyoathiriwa na vurugu, ukosefu wa usalama na viwango duni vya usalama inapaswa kuwa sawa kote Kenya. Ni sharti tuache mazoea ya dhana kwamba kuna matokeo tofauti ya vurugu katika sehemu tofauti ya nchi. Kufanya mabadiliko haya kunahitaji usawa katika usambazaji wa maafisa wa polisi, mashtaka na juhudi za kuzuia uhalifu.

2. **Mkakati wa Usalama wa Kitaifa unaojivuniwa na raia** — Baada ya kugundua kuwa usalama ni wa raia, tunahitaji mbinu inayozingatia usalama wa kibinadamu iwekwe katika Mkakati kamili wa Kitaifa wa Usalama na Ulinzi (kila baada ya miaka miwili na kila Rais anayeingia mamlakani katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuchukua hatamu za uongozi) na ambayo inamilikiwa na watu na serikali yote. Inapaswa kuwa amilifu, yenye kuzuia, na ya kutahadharisha.

3. **Kutoathiriwa sana na migogoro ya rasilimali, majanga, dharura na uhaba wa chakula** kwa kutekeleza Mkakati kamili wa Dharura za Kitaifa, Mkakati wa Kushughulikia Maafa na Migogoro uliowekwa kwenye sheria ambayo inahusishwa na mipango ya kukabiliana na majanga katika ngazi ya kaunti, kaunti ndogo na wadi ambayo husasishwa mara kwa mara**.**

4. Ugaidi ni tishio linaloendelea kuathiri Wakenya ambao wanahitaji zana mbalimbali kulishughulikia, si usalama tu - Kukabiliana na Ugaidi kutafanikiwa tu ikiwa utahusishwa zaidi na ulinzi wa kisiasa, kijamii na

kitamaduni ambao hupunguza idadi ya wanaosajiliwa, na kutohalalisha malengo ya maadui wetu.

i. Kuangazia na kuratibisha mipango ya kuzuia itikadi kali na mafunzo yanayochochea vurugu katika Wizara zinazohusika na afya, elimu, vijana, utamaduni na turathi.

ii. Kuhusu namna Fedha za Kulinda Waathiriwa zinavyotumiwa, waathiriwa wa ugaidi wanapaswa kupewa kipaumbele kwa kuwa kunyanyaswa kwao kunalenga kutishia Wakenya wote moja kwa moja pamoja na viongozi tuliochagua kwa misingi ya kisiasa, kijamii na kidini.

5. **Masuala ya Kigeni**— Kutathmini mahusiano ya kidiplomasia na mataifa yanayofadhili ugaidi, misimamo mikali ya kidini, na upanuzi au kujitenga Hakikisha diplomasia imeundwa na kufadhiliwa ili kukabiliana na vitisho vinavyoibuka kabla ya kudai mwitiko madhubuti wa usalama. Kuhusiana na bajeti, ni muhimu kwamba Wizara ya Masuala ya nje, inapata mgao sawa na Idara ya Ulinzi, Huduma ya Kitaifa ya Ujasusi (NIS), na vyombo vingine vya usalama.

6. **Utendakazi wa polisi, na afya ya akili na ustawi -** Kuimarisha utendakazi na huduma za Shirika la Huduma za Kitaifa za Polisi, pamoja na kuboresha afya ya akili na ustawi wa maafisa hao.

i. Fafanua Viashiria Muhimu vya Utendakazi kwa makamanda wa polisi kutoka katika ngazi ya Inspekta Jenerali wa Polisi hadi chini kwa kitengo cha umma cha kuripoti takwimu za uhalifu wa kitaifa na ukosefu wa usalama. Vitengo hivi viwili vizingatiwe katika kupandisha vyeo na kutoa vivutio.

ii. Unga mkono maadili na utendakazi bora katika NPS kwa kutambua na kutuza ufanisi, kujituma na kujitolea kwa maafisa na wananchi.

iii. Kama suala la kipaumbele, pawe na huduma za ushauri kuhusu afya na matibabu ya akili ya maafisa wa polisi. Polisi walio na majukumu makubwa ambayo yanawaweka katika hatari ya

kudhurika kiakili wapewe mazingatio maalum. Hatua zote zinapaswa pia kuchukuliwa ili kuweka familia pamoja.

**7. Linda Wananchi dhidi ya vitisho vya kibinafsi na hatari**

i. Kukabiliana na visa vya unyanyasaji wa kijinsia na ngono kupewe kipaumbele kwa kuzingatia na kutoa rasilimali maalum kwa polisi na kuchukua hatua za kuzuia dhuluma za kijinsia na ngono.

ii. **Shughulikia mizozo ya mipaka ambayo inahatarisha usalama wa kitaifa na jamii -** Unda tume maalum au majopokazi kwa kila mzozo wa mpaka ili washauriane na wadau wote na kutoa mapendekezo ya mageuzi ambayo yatashughulikiwa.

iii. **Wafichuzi wa uhalifu walindwe** — Wezesha taratibu za mahakama ambazo zitahakikisha usalama na ulinzi wa watoaji habari, wafichuzi na mashahidi, hususan wa ugaidi, uhalifu mkubwa wa kimataifa, na ufisadi.

iv. **Utatuzi wa migogoro inayokumba wananchi -** Imarisha ujuzi wa raia wa kutatua migogoro na upatanishi katika mfumo mzima wa elimu ya Kenya. Fanikisha hili kwa kujumuisha maarifa ya utatuzi wa migogoro, mazungumzo na ushauri katika mtaala wa elimu katika ngazi zote za elimu ya msingi na sekondari.

v. Linda Wakenya dhidi ya vyakula hatari kwa kuimarisha usimamizi wa usalama wa chakula.

# Sura ya 11 — Tume na Masuala Yanayogusa kila kipengee

1. Tenganisha kazi ya kuchunguza makosa ya uhalifu na ile ya kupandisha vyeo na kuhakikisha maadili yamezingatiwa katika utumishi wa umma. Kazi ya kuripoti kuhusu kupandisha vyeo na utekelezaji wa maadili itafanywa na Tume iliyopendekezwa ya Maadili inayozungumziwa katika sura ya maadili ya kitaifa.

2. Bainisha majukumu ya mashirika ya udhibiti ili kuhakikisha kwamba hakuna urudiaji wayo, na kurahisisha uwazi, pawe na huduma za haraka zinazopatikana gharama nafuu ili sheria ya udhibiti ifuatwe kwa viwango vya juu.

3. Kuimarisha Maabara ya Serikali ili kuifanya iwe imara katika utekelezaji wa majukumu yake.

4. Unda taasisi madhubuti iliyoungana ya kudhibiti na kuhakikisha usalama wa chakula.

5. **Kaunti ya Nairobi –** Ni kaunti tofauti na nyingine kutokana na ukweli kwamba ndio mji mkuu wa taifa ulio na ofisi za Umoja wa Mataifa (UN). Ofisi za UN jijini Nairobi ni makao makuu ya tatu ya Umoja huo ulimwenguni. Ndio sababu ni tofauti na kaunti nyingine. Wakenya wanaustahi mji huu mkuu kuwa wenye vitengo vyote vikuu vya Serikali na kama eneo muhimu kwa ushiriki wao wa mijadala ya uraia katika maisha ya kitaifa. Hii ina maana kuwa Tume ya Ugavi wa Mapato inaweza kujitahidi kuzingatia hadhi hii maalumu ya Nairobi na mahitaji ya huduma ambayo huja nayo.

   Zaidi ya kuuzingatia kama mji mkuu, makubaliano ya tarehe 26 Machi 1975 kati ya Jamhuri ya Kenya na Umoja wa Mataifa kuhusiana na makao makuu ya Shirika la Umoja wa Mataifa

kuhusu Mazingira jijini Nairobi yanabainisha hatua za Serikali ya Kitaifa kuboresha mazingira, miundo msingi, huduma za umma, na ufikiwaji wa makao makuu haya. Hatua hizi zinakubaliwa na Serikali ya Kitaifa na si Serikali ya Kaunti. Hadhi ya Nairobi kama mwenyeji wa makao makuu ya Umoja wa Mataifa ni sababu kubwa ya kuwa kitovu cha kidiplomasia ambapo nchi kadhaa huanzisha ujumbe maalum ambao huruhusu uwakilishi katika UNEP na mashirika mengine ya UN yanayoendeshwa kutoka Nairobi. Jopokazi linapendekeza kwamba Nairobi ipewe hadhi maalum ya mji mkuu ambao unaipa Serikali ya Kitaifa njia ya kutoa huduma na uwezeshaji ufaao katika kuudumisha kama mji mkuu na kama kitovu cha kidiplomasia. Kwa wakati huo huo, hadhi maalum kama hiyo haifai kuzuia haki za wakazi wa Nairobi za uwakilishwaji katika ngazi za wadi na bunge.

6. **Kuteua Makamishna wa IEBC** — Mkutano wa Viongozi wa Vyama Kisiasa Bungeni utateua kwa makubaliano, watu watakaopendekezwa kuteuliwa na Rais kama makamishna wa IEBC. Wanaosaka nafasi hiyo wanapaswa kufikia vigezo vilivyoainishwa katika Katiba na sheria na hawapaswi kuegemea upande wowote, na rekodi ya uadilifu na mambo walioyaafiki, na ambao si wanachama maarufu wa chama cha kisiasa na hawana rekodi ya kuchukua nafasi za umma kwa msaada ya chama.

7. **Makamishna wa muda** — Nusu ya Makamishna katika Sura ya 15 kuhusu Tume, isipokuwa kwa IEBC, wanapaswa kuhudumu kwa muda maalum.

8. Ni sharti kila tume huru iwe na mifumo ya ndani ya uwajibikaji ambayo hutenganisha kwa njia huru na wazi mamlaka ya uteuzi na kupandisha vyeo na yale ya kusimamisha kazi na kusuta.

9. Ukaguzi mkali wa mahesabu unaochunguza thamani ya matumizi ya pesa na kuendeleza kanuni bora za usimamizi wa fedha za

umma unapaswa kutumika katika kila kitengo cha serikali na kila asasi ya umma.

10. Kifungu cha 249 (3) kimekiukwa na hii imeathiri uwezo wa Tume za Sura ya 15 na ofisi huru kutekeleza ipasavyo na kwa njia huru majukumu yao. Wakati huo huo, Tume na ofisi huru pia zinapaswa kupitia ukaguzi mkali na mashirika yafaayo ili kuhakikisha kuwa zinatimiza majukumu yao kama inavyotakiwa.

11. **Jumuisha mabaraza ya usimamizi -** Hivi sasa, karibu kila sheria huanzisha mamlaka fulani ya udhibiti au nyingine pia hubuni baraza fulani la rufaa kusuluhisha mambo yanayotokana na zoezi la wadhibiti wa mamlaka yake ya kisheria. Uhusiano kati ya mdhibiti na mabaraza haya umekosesha maana mantiki ya hukumu zisizoegemea upande wowote katika kuamua mizozo. Isitoshe, idadi kubwa ya mabaraza ya hukumu yaliyobuniwa kwa njia huishia kufuja rasilimali za kitaifa pakubwa. Inapendekezwa kuunda Baraza Moja la Rufaa ya Kitaifa ambalo litasikiza na kuamua kesi tofauti za rufaa (kama vile, nguvu na kawi, michezo, na mazingira).

12. Punguza idadi ya mashirika ya udhibiti kwa kufanya juhudi kubwa za kurahisisha uoanishaji na majukumu yao. Lengo ni kuwa na kanuni chache na zenye kutekelezwa kwa njia bora, na zawadi dhidi ya rushwa katika mchakato huu.

***Jopokazi linapendekeza kwamba wananchi wachukue muda kusoma ripoti nzima ambayo ina mitazamo muhimu na mapendekezo zaidi.***